KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 14, Issue 5

02nd Dhul Qa'dah 1432

30th Sept, 2011

YALIYOMO

HADEETH YA TAMEEM AD-DAARI (رضي الله عنه) **MASEEH AD-DAJJAAL** 1 - 3

Na: Sheikh A. Hijazi (حفظه الله)

HADEETH KUMUHUSU AL-JASSAASAH

[*Al-Jassasah ni mnyama mwenye manyoya mingi sana; amejaa manyoya kiasi cha kwamba utashindwa kumpambanua mbele yake kutokamana na nyuma yake*]. Amepokea Imaam Muslim yakwamba Amir Bin Shurahil alimuuliza Fatimah bint Qais, dadake Adh-Dhahhak bin Qais, aliyekuwa ni miongoni mwa (Waislamu Wanawake) wa kwanza waliohama (kuelekea Madinah), "Hebu nisimulie nami hadeeth ambayo uliyowahi kuisikia wewe mwenyewe moja kwa moja kutoka kwake Mtume (صلى الله عليه وسلم), na si mwengine yoyote." Akasema (Fatimah), "Nitafanya hivyo, ukitaka." 'Amir akasema, "Na'am tafadhali, nieleze." Akasema, "Mimi niliolewa na mtoto wa Al-Mughirah, ambaye aliyekuwa ni miongoni mwa vijana bora wa ma-Quraish. Aliwahi kujeruhiwa (katika vita vya kwanza) vya Mtume (صلى الله عليه وسلم) [akiwa katika upande wa Mtume].

NENO LA BUSARA

Amesema Hudhayfah bin Al-Yaman, "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisimama mbele yetu na hakuacha tukio (kubwa) lolote (litakalotokea mbeleni) bila kulitaja,mpaka mwanzo wa qiyaamah.Kuna wale waliyokuwa na 'ilmu juu yake, na kuna wale wasiyokuwa na 'ilmu juu yake.Baadaye nitasahau jambo(katika matukio yatakayotokea mbeleni aliyoyasikia kutoka kwa mtume), na nitalikumbuka, kama mtu anavyomkumbuka mtu aliye mbali na yeye.Humuona na kumkumbuka."(Imepokewa na Bukhaaree & Muslim).

Nilipotalikiwa [Al-Mughirah alimuacha kama alivyopokea Imaam Muslim katika swaheeh yake] 'Abdur-Rahmaan bin Awf akifuatana na baadhi ya Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuja kuniposa. Vilevile Usamah bin Zaid alitaka kuniposa. Kabla ya hapo niliwahi kuambiwa yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Yoyote anipendae mimi, basi na ampende nae Usamah." Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuwa akizungumza na mimi, nikamwambia '(Mas'ala ya) kuhusiana na posa zangu iko kwenye mikono yako, kwahivyo, nioze mimi kwa umtakae." Akasema, 'Basi nenda ukakae kwenye nyumba ya Umm Shiraik.' Umm Shuraik alikuwa ni miongoni mwa Answaar. Alikuwa akitoa sana kwa njia ya Allaah. Vilevile, nyumba yake ilikuwa haishi wageni kila saa. Nikasema, "Haya, mimi nitafanya hivyo usemavyo.' Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema, 'Laa usifanye hivyo. Umm Shuraik ana wageni wengi sana, na mimi nachukia isije *khimaar* yako ikakuanguka, au kwamba nguo yako (kwa bahati mbaya) ikapigwa na upepo na kuonyesha miguu yako, baadhi ya watu (watakaokuwa hapo) hwenda wakakuona kwenye sehemu usopenda kuonekana. Nenda ukakae kwenye nyumba ya binamu yako, Abdullaah bin Amr bin Umm Makhtoom [aliekuwa kipofu]. Alikuwa ni mtu kutoka Fihr, kabila la ki-Quraish. Alikuwa ni katika kabila lake (Fatimah). 'Basi nikaingia pamoja nae (kama mgeni). Nilipomaliza *iddah* yangu, nilimsikiya mpiga mbiu wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akiwatangazia (Waislamu waje msikitini), mimi nikakaa kwenye mstari wa wanawake uliokuwa nyuma baada ya mstari wa wanaume. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipomaliza kuswalisha, alikaa kwenye *minbar* na huku akiwa anacheka. Kisha, akasema: "Kila mmoja wenu na akae mahali alipokuwa akiswali." kisha akasema, "Je mwajua sababu ya kuwakusanya hapa leo?" wakasema, "Allaah na Mtume wake ndio wajuao." Akasema, "Wallaahi, mimi sikuwakusanya kwa ajili ya kuwachochea au kuwaonya. Kinyume chake, mimi nimewakusanya kwa sababu Tameem ad-Daari, ambaye ni *mkristo*, aliyenijia kusilimu na kunipa *baiy'ah*, alinitolea kisa kinachofanana na niliyokuwa nikiwaeleza hapo awali kumuhusu Maseeh Mrongo. Aliniambia yakwamba alipanda Meli na kusafiri nayo kwenye Bahari, akiwa pamoja na watu thalathini katika (makabila ya) Lakhm na Judham [haya ni makabila mawili kutoka Yemen]. Mawimbi makali yakakiangamiza chombo chao kikapanda mwamba kwa muda wa mwezi mzima mpaka, kulipokurubia kuchwa kwa jua, wakalazimika kutua karibu na kisiwa kwenye bahari. Kwahiyo, wakapanda mashuaokozi wakatua kwenye kisiwa ambapo walikutana na mnyama aliyekuwa na manyoya mingi sana. Alikuwa amejaa manyoya kiasi cha kwamba utashindwa kumpambanua mbele yake kutokamana nyuma yake." Wakasema, 'Ole wako! Wewe ni nani?' Akajibu, 'Mimi ni *Al-Jassaasah*.' Wakasema, 'Na ni kitu gani hicho *al-Jassaasah*?' Akajibu, 'Enyi watu! Ingieni kwa huyu mtu aliye ndani ya Hekalu, kwani yeye anawasubiri kwa hamu sana kutaka kujua habari zenu.' Akasema, 'Alipotutajia sisi mtu, tulihofiya yakwamba yeye alikuwa ni Shetwani.' Kisha akasema, 'Tukamuondokea kwa haraka. Kisha tukaingia ndani ya Hekalu. Hapo ndani palikuwa na Jitu kubwa ambalo hatujawahi kuona mfano wake, akiwa amefungwa na Mijisili-sili mikubwa ya ajabu. Mikono yake ikiwa imefungwa kwenye shingo yake. Alikuwa (amefunikwa) na silisili za chuma

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

kuanzia kwenye magoti yake mpaka kwenye visigino vyake. Tukasema, “Ole wako! Wewe ni nani?” Akatujibu, “Mutapata habari zangu huvi karibuni, lakini kwanza hebu nipasheni habari, nyinyi ni kina nani?” Wakasema, “Sisi ni watu wa kabila la Waarabu. Tulipanda Meli tukasafiri nalo katika wakati ambapo bahari ilikuwa imechafuka. Mawimbi makali yakakiangamiza chombo chetu kikapanda mwamba kwa muda wa mwezi mzima. Kisha tukafika kwenye kisiwa chako. Tukapanda mashuaokozi mpaka hatime tukafika kwenye kisiwa. Tukakutana na Mnyama aliekuwa amejaa manyoya kiasi cha kwamba utashindwa kumpambanua mbele yake kutokamana na nyuma yake.” Tukasema, “Ole wako! Wewe ni nani?” Akatujibu, “Mimi ni al-Jassaasah.” Tukasema, “Na ni kitu gani hicho *al-Jassaasah*?’ Akajibu, “Ingieni kwa huyu mtu aliye ndani ya Hekalu, kwani yeye anawasubiri kwa hamu sana kutaka kujua habari zenu. Basi tukaja kwako kwa haraka kwa sababu tulikuwa na khofu nae na tukaogopa yakwamba huwenda akawa ni Sheitwani.” Akasema (yule mtu aliyefungwa na silisili), “Hebu nielezeni kuhusu Miti ya mitende iliyoko Baisan” [kijiji kilichoko nchini Jordan]. Tukamjibu, “Wataka kujua nini kuhusu mitende hiyo?” Akasema, “Mimi nawauliza kuhusu mitende yake, bado yanatoa mazao?” Tukasema, “Na’am, ndio.” Akasema, “Hivi karibuni hayatotoa mazao yake!” Kisha akasema, “Hebu nielezeni kuhusu mto wa Taberias [bahari ya Galilee]. Tukasema, “Wataka kujua nini kuhusiana na mto huo?” Akasema, “Kwani bado mto huo una maji?” Tukamjibu, “Una maji mengi sana.” Akasema, “Maji yake yatapotea hivi karibuni.” Kisha akasema, “Hebu nielezeni kuhusu Chemchemi ya Zughar [Kijiji katika nchi ya Syria].” Tukasema, “Wataka kujua nini kuhusu Chemchemi hiyo?” Akasema, “Bado mkondo wake wa maji unapita na watu wake bado wanapanda mimea kwa kutumia maji yake?” Tukasema, “Na’am. Bado mkondo huo umajaa maji, na watu wake bado wanaendelea kupanda mimea kwa kutumia maji yake.” Akasema, “Hebu nielezeni yaliyojiri kumuhusu Mtume wa wasiojua kusoma wala kuandika [waarabu].” Wakasema, “Alihama kutoka Makkah na kuelekea Yathrib [Madinah].” Akasema, “Je, Waarabu washampiga vita?” Tukasema, “Na’am.” Akasema, “Kisha akawafanya nini?” Tukamwambia yakwamba aliwashinda hao Waarabu waliokuwa karibu yake [karibu na Madinah] kisha wakamfuata.” Kisha akawauliza, “Lakini ni kweli yakuwa haya yashatokea?” Tukamjibu, “Na’an, ni hakika.” Akasema, “Ingelikuwa ni bora kwao lau kama wangelimfuata. Sasa nitawaeleza mimi ni nani. Mimi ni Maseeh (Maseeh wa urongo). Hivi karibuni, nitaruhusiwa kujitokeza. Nitaondoka hapa nitembee katika kila sehemu ya ardhi hii. Mimi sitowacha kijiji chochote isipokuwa nitapenya, kwa muda wa siku arubaini, isipokuwa Makkah na Taiybah (Madinah), kwani mimi nimeharamishiwa kuiingia Miji hiyo. Kila nitakapojaribu kuiingia mojawapo ya miji hiyo, nitakutwa na Malaika akiwa ameuinia upanga juu, kwahiyo atanizuiya (kuingia) Miji hiyo. Katika kila mlango wake, kutakuwa na Malaika waliosimama kulinda sehemu hizo.’”

Kisha (Fatimah bint Qais) akasema: “Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema na huku akiigonga *minbar* kwa fimbo yake, ’Hii ni Taiybah! Hii ni Taiybah!’ Kumaanisha Madinah. ‘Je, mimi sikuwasimulia (kisa) kama hicho?’ Wakajibu, ‘Na’am, ni hakika.’ (Kisha akasema), ‘Nimependezwa na aliyonieleza Tameem ad-Daari. Yanakubaliana na niliyowaambia kumuhusu (Maseeh wa urongo), Madinah, na Makkah. Yeye yupo kwenye bahari ya Ash-Shaam [hizi ni sehemu za kushikana kuanzia kaskazini mwa Uarabuni mpaka Anatolia nchini Uturuki, na kuanzia kwenye mto wa Euphrates mpaka mwambao wa Mashariki ya bahari ya Mediterranean. Sasa hivi inahusisha nchi ya Syria, Jordan, Palestina na Lebanon], au Bahari ya Yemen. Laa! Kwa hakika yeye yupo kwenye sehemu za Mashariki (ya Madinah). Kwa hakika ni katika sehemu ya Mashariki, Kwa hakika ni katika sehemu ya Mashariki.” Na akaashiriya kwa kuelekeza kwa mkono wake katika upande wa Mashariki. Akasema (Fatimah), Na mimi nimeihifadhi hadeeth hii kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Katika hadeeth hii, kulirudia na kulikariri neno “Kwa hakika” inaashiriya kuthibitisha kwa uhakika, yakwamba Maseeh wa urongo atatokeza kutoka upande wa Mashariki ya Bahari ya Maditerrenean (Iraq na sehemu zilizoko upande wake wa Mashariki).

AD-DAJJAAL NI MYAHUDI

Amepokea Imaam Muslim yakwamba Abu Sa’eed al-Khudhree amesema: “Ibn Sa’eed ameniambia, nilipokuwa na wasiwasi nae, “Mimi nimejitahidi kadiri ya uwezo wangu na watu (katika kuwashawishi yakwamba mimi sie ad-Dajjaal), bila ya kufaulu! Matatizo baina yangu mimi na nyinyi ni nini, enyi Maswahaba wa Muhammad! Kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakusema yakwamba “Yeye ni Myahudi?”, na mimi nimesilimu. Vilevile akasema, “Hatokuwa na watoto.” na mimi niko hapa sasa, na watoto wangu. Pia alisema, “Allaah alimuharamishia kuingia Makkah na Madinah ...” [*Muslim. Sharh an-Nawawee ‘alaa swaheeh Muslim vol. 18 Uk. 79-83*]

Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akishuku yakwamba Ibn Sa’eed ndiye aliyekuwa ad-Dajjaal alipokuwa bado ni mdogo. Hii ni kwa sababu Ibn Sa’eed alikuwa akijishughulisha na mambo ya Majini. Pia alikuwa akidai yakwamba habari za *Ghaib* (zenye kufichikana) zilikuwa zikimfikia yeye na kwamba alikiona Kiti juu ya Bahari, kiti cha Iblisi. Lakini hata hivyo, baadae alisilimu.

Abu Sa’eed al-Khudhree amewahi kuonana na Ibn Sa’eed mara nyingi. Akasema, “Niliwahi kuwa na Ibn Sa’eed wakati fulani kwa ajili ya kutekeleza Hajj katika Mji wa Makkah. Akaniambia, “Mimi nimesumbuliwa na watu kwa sababu wamedai yakwamba ati mimi ni ad-Dajjaal. Kwani wewe hukuwahi kumsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema, “Yeye (ad-Dajjaal) hatokuwa na watoto?” nikamjibu, “Na’am, ndio.” Akasema, “Mimi niko hapa, na nina watoto. Kwani wewe hukuwahi kumsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema, hatoingia Madinah wala Makkah?” Nikamjibu, “Mimi nimwzaliwa Madinah na sasa hivi mimi niko hapa naelekea Makkah.” Kisha (Abu Sa’eed) akasema, “Kisha maneno yake ya mwisho kwangu alisema, “Wallaahi! Mimi najua siku alipozaliwa, mahali alipozaliwa, na pale alipo hivi sasa!” Kisha (Abu Sa’eed) akasema, “Huyu (Ibn Sa’eed) amenitatiza na kunikanganya.” Vilevile, amepokea Imaam Muslim yakwamba Abu Sa’eed al-Khudhree amesema: “Tulikwenda Hajj au Umrah pamoja na Ibn Sa’eed. Tukapumzika kwenye sehemu ambayo watu (kundi la msafara) wametawanyika kila mahali (kwa mapumziko) na mimi nikabaki peke yangu na Ibn Sa’eed. Nikawa na wasiwasi kutokana na wasemayo watu kumuhusu yeye. Akaja na mzigo wake na kujipumzisha ubavuni mwa mizigo yangu.

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Nikasema, “Ah, kuna joto sana! Kwanini huwendi chini ya ule mti ukaweka mzigo wako?” Akafanya hivyo, kisha kukapita kundi la kondoo karibu yetu. Akaondoka , mara akaja na kombe kubwa (la Maziwa), akasema, “Kunywa, Ewe Abu Sa’eed! Nikasema, “Kuna joto sana na hayo Maziwa ni moto!” Sikutaka kunywa kutoka kwenye mkono wake, au kupokea kutoka kwenye mkono wake. kisha akasema, “Ewe Abu Sa’eed! Nilikurubia kufikiria nichukuwe kamba niilweleweshe kwenye mti ili nijitie kitanzi kwa sababu ya wanayoyasema watu kunihusu mimi. Ewe Abu Sa’eed! Ni nani aliyekuzidi wewe katika ’ilmu ya hadeeth za Mtume (صلى الله عليه وسلم), Ewe Answaar? Kwani wewe si miongoni mwa walio bora katika ’ilmu ya Hadeeth za Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakusema yakuwa, Yeye (ad-Dajjaal) ni Kaafir? Hatahivyo, mimi ni Muislamu. Kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakusema yakuwa atakuwa Tasa? Mimi nimewawacha wanangu Madinah.Kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakusema yakuwa hatoingia Makkah wala Madinah, sasa hivi mimi natoka Madinah na naelekea Makkah.” Abu Sa’eed akasema nikakurubia kumuhurumia. Kisha akasema, “Wallaahi! Mimi namjua (ad-Dajjaal), mahali alipozaliwa na mahali alipo hivi sasa!” kisha (Abu Sa’eed) akasema: “Nikamwambia, Ole wako katika siku iliyobaki.’”

Kinachothibitisha yakwamba ad-Dajjaal ni Myahudi ni kwamba, pindi atakapojitokeza katika Mji wa Asfahaan, [Sehemu za Khurasaan], vilevile kunaitwa Asbahan, Mayahudi Elfu Sabiini watamfuata.

Anas Bin Maalik amepokea yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم) Mayahudi wa Asbahan Elfu Sabiini, wakiwa wamevaa vikashida, watamfuata yeye (ad-Dajjaal).

KUANGAMIA KWA AL-MASEEH AD-DAJJAAL

Kama ilivyopokewa katika hadeeth nan an-Nawwaas bin Sam’an, ad-Dajjaal atauwawa na ’Eesa, mwana wa Maryam. Kifo cha ad-Dajjaal kitatokea baada ya Malaika kumgeuza aelekee ash-Shaam mbali na pambizoni mwa Madinah. Atatokomea ash-Shaam karibu na Mlango wa Mashariki wa Ludd, nchini Palestina, Twamuomba Allaah Awarudishie Waqislamu Nchi yao. Ameen! Ameen! Ameen!

THE QUR’AN & SUNNAH HAJJ / ’UMRAH AGENCY

1432HIJRI/ 2011 C.E

Assalaamu ‘Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh:

Tunafuraha kuwajulisha yakwamba Insha Allaah mwaka huu 1432 Hijri/ 2011, tumeanza Barnaamij ya kupeleka watu Hajj.

Mipangilio Ya Safari

- Kuondoka ni katika wiki ya mwisho ya mwezi wa Dhul Qa’dah
- Kurudi ni mwisho wa mwezi wa Dhul-Hijjah
- Safari itaanza Mombasa – Nairobi – Jeddah
- Kurudi ni Jeddah – Nairobi – Mombasa
- Gharama ya Safari (ikiwemo Hoteli, Usafiri na Chakula – mara 3 kwa siku tukiwa Mina kwa siku tano)
- Class “B” ni $3800 U.S Dollars / Class “C” ni $3200 U.S Dollars
- Amma mas’ala ya Chakula (Makka na Madinah) kila mtu ni juu yake
- Tutakuwa na Darsa juu ya mas’ala ya Hajj kabla ya kuondoka na tutakapokuwa Makkah
- Tutaandamana na Daktari wetu kutoka hapa Mombasa Insha Allaah

Kwa Maelezo Zaidi

Fika katika Maktaba ya QSS iliyoko ubavuni mwa Tajj Hotel (Duka la tatu baada ya Duka la vitabu vya Dini), au

Wasiliana nasi kwa kutuandikia barua Pepe kwa info@qssea.net, au

Tupigie simu nambari mojawapo ya hizi zifuatazo:

+254 723471820 au +254 721473181, au +254 700365253

(Continued from Vol 14, Issue 4)

Kujilinda Na Fitnah Ya Dajjaal

Mtume (صلي الله عليه وسلم) amewafunza ummah wake namna ya kujilinda na fitnah ya Maseeh mrongo ad-Dajjaal, ameuacha ummah wake katika njia ilio wazi, na hakuna apoteaye kutoka katika njia hiyo ila yule aliyeangamia.

Hakuacha jambo zuri ila amewaonyesha ummah, au jambo baya bila ya kuwaonya wao. Baadhi ya mambo aliyotuonya nayo ni fitnah ya ad-Dajjaal, kwa sababu ndio fitnah kubwa ummah utakao kumbwa nayo mpaka kitakaposimama Kiyama. Killa Mtume alionya watu wake kuhusu chongo ad-Dajjaal, lakini Muhammad (صلي الله عليه وسلم) ndie aliyeonya watu wake zaidi kumuhusu yeye. Allaah (سبحانه وتعالى) alimsifia Mtume (صلي الله عليه وسلم) sifa zake nyingi ili aweze kuwaonya watu wake. Bila shaka ad-Dajjaal atajitokeza kwa ummah huu, kwa sababu ni ummah wa mwisho. Na Muhammad (صلي الله عليه وسلم) ndie Mtume wa mwisho.

Inayofuata ni taratibu ya baadhi ya aliyotuwekea mteule wetu Mtume (صلي الله عليه وسلم) ili iwe ni kinga na fitnah hii kubwa. Kutoka kwayo (hio fitnah) twamuomba Allaah atuhifadhi na atupe ulinzi wake:

◊ Kubakia kwenye Uislamu, kuwa na imani iliyo swaheeh na kujifunza Majina na Sifa nzuri za Allaah (سبحانه وتعالى) ambazo hashirikiani na yoyote. Yatakikaniwa ifahamike kuwa ad-Dajjaal ni binadamu atakayekula na kunywa, na Allaah (سبحانه وتعالى) Yuko mbali na hayo. Ad-Dajjaal atakuwa chongo lakini Allaah (سبحانه وتعالى) si chongo; hakuna atakayemuona Mola wake mpaka afe, lakini ad-Dajjaal ataonekana na watu wote, waumini na makafiri kwa jumla atakapojitokeza

◊ Kujilinda kwa Allaah (سبحانه وتعالى) na fitnah za ad-Dajjaal, haswa katika swala. Hii imehadithiwa katika hadeeth swaheeh, kama ile iliyohadithiwa kutoka kwa Umm al-Mu’mineen Aa’ishah (رضي الله عنها), mke wa Mtume (صلي الله عليه وسلم) aliesema kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alikuwa akiomba katika swala yake *“Allahuma inni a’oodhubika min ‘adhaab al-qabri, wa a’oodhubika min fitnat il-maseeh il-dajjaal, wa aoodhu bika min fitnat il-mahyaa wa fitnat il-mamaat. Allahumma inni a’oodhu bika min al-ma’tham wa’l- maghram.”* (Yaa Allaah najilinda kwako kutokana na adhabu ya kaburi, na jilinda kwako na fitnah ya ad-Dajjaal, na najilinda kwako na fitna ya maisha na kifo. Yaa Allaah najilinda kwako na madhambi na deni.” **[al-**

(Continued from page 3)

Bukhari no.789]

◊ Abu Hurairah - Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: "Yeyote atakaesema Tashahhud (katika swala) basi na ajilinde na mambo manne-(kama ijulikavyo adhabu ya kaburi-fitnah ya ad-Dajjaal-fitna ya maisha na kifo- **Muslim no.924).**

◊ Kuhifadhi aya zilizo Sura al-Kahf. Mtume (صلي الله عليه وسلم) ametuhimiza kusoma ufunguzi wa sura al-Kahf, yakuhifadhi na ad-Dajjaal kulingana na baadhi ya riwaya, aya za mwisho zilitajwa kuhusu sura hii. Hii yamaanisha kusoma aya kumi za mwanzo au kumi za mwisho. Miongoni mwa hadeeth inayotaja hizi ni hadeeth ndefu ya al-Nawwaas ibn Sam'aan (رضي الله عنه) ambayo yasema: "yoyote katika nyinyi mkimuona (ad-Dajjaal) soma dhidi yake ayaat za mwanzo wa sura al-Kahf." **(Muslim no.5228)**

Kutoka kwa Abu'l Dadaa' kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: "Yeyote aliyehifadhi aya kumi za mwanzo wa sura al-Kahf atahifadhiwa kutokana na ad-Dajjaal"-yaani kutoka kwa fitnah yake. Muslim alisema "Shu'bah alisema kutoka mwisho wa al-Kahf.' Hammaam alisema, kutoka mwanzo wa al-Kahf."'

Al-Nawawi **(sharh Muslim, 6/93)** alisema: "sababu ya hii ni kwa sababu mwanzo wa sura hii, imetajwa miujiza na dalili, na yoyote anaezizingatia hatodanganyika na fitnah ya ad-Dajjaal. Na mwisho wa sura hii Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **[Je! Wale waliokufuru wanadhani yakwamba kule kuwafanya waja wangu kuwa walinzi (wao) badala yangu (kutawafaa kitu kufanya hivyo?) Hakika Sisi tumeandaa Jahanamu iwe ndipo mahala pa kuteremkia makafiri. [AL-KAHF 18: 102]."**

Hii ni alama maalum katika sura al-Kahf. Kuna hadeeth zenye kuhimiza kuisoma, haswa siku ya Ijumaa.

Al-Haakim kutoka kwa Abu Sa'eed al-Khudree' (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: "Yeyote atakayesoma surat al-Kahf siku ya Ijumaa, itakuwa muangaza kwake kutoka Ijumaa moja hadi nyengine." **[al-Mustadrak, 2/368. Swaheeh al-Jaami' as-Swagheer, no.6346]**

Bila shaka sura ya al-Kahf ina umuhimu sana na ni yenye aya tukufu, kama kisa cha watu wa pango, kisa cha Musa na al-Khidr (عليهم السلام), kisa cha Dhu'l-Qarnayn (عليه السلام) na kujenga kwake bwawa kuwazuia Ya'jooj na Ma'jooj, ushahidi wa kufufuliwa na kupulizwa kwa tarumbeta, na maelezo ya matendo ya wale waliopotea mno, wale wanaofikiri kuwa wameongoka ili hali wamepotoka na ni vipofu. Kila Muislamu atakakiwa afanye juhudi kuisoma sura hii. Na kuihifadhi na kuisoma kwa kuirudia, haswa siku iliyo bora ya kuchomoza kwa jua, nayo ni Ijumaa.

KUMKIMBIA ad-DAJJAAL NA KUKAA MBALI NAYE

Njia iliyo bora ni kukaa Makkah au Madeenah, na sehemu ambazo ad-Dajjaal hatoingia. Ad-Dajjaal atakapojitokeza, Waislamu watatakiwa wakae mbali naye, kwa sababu ya atakavyowatatiza watu na miujiza atakayokuwa nayo, ambayo Allaah (سبحانه وتعالى) atajaalia iwe mikononi mwake ili kuwajaribu binadamu. Mtu atakuja kwake, akidhani kuwa yeye ni mu'min wa nguvu, kisha amfuate ad-Dajjaal. Twamuomba Allaah atuhifadhi na fitnah zake.

Imraan ibn Husayn kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: "Yeyote atakaesikia kuhusu ad-Dajjaal, basi na akae mbali naye, kwakuwa mtu atamjilia yeye akidhania kuwa asema ukweli kwa sababu ya miujiza aliotumwa nayo." **[Imaam Ahmad no.19118, Abu Dawood no. 3762 na al-Haakim 4/31]**

Kifo Cha ad-Dajjaal

Ad-Dajjaal atakufa mikononi mwa Maseeh 'Eesa Ibn Mar'yam (عليه السلام) kama ilivyobashiriwa na hadeeth swaheeh. Ad-Dajjaal atajidhihirisha katika ardhi na atakuwa na wafuasi wengi, akitambaza fitnah yake kwa marefu na mapana. Hakuna atakayenusurika na fitnah ila waumini kidogo, wakati huo, Eesa ibn Mar'yam (عليه السلام) atateremka upande wa mnara wa mashariki Damascus, na waja wa Allaah waumini watakusanyika kwake. Atawaongoza kumuendea ad-Dajjaal ambaye wakati wa kuteremka Eesa atakuwa anaelekea Bayt al-Maqdis. Eesa atamkurubia katika mlango wa Ludd katika mji wa Falestina karibu ya Bayt al-Maqdis, ad-Dajjaal atakapomuona, ataanza kuyayuka kama chumvi katika maji, lakini Eesa (عليه السلام) atamwambia: "Nina shughuli nawe hutonikimbia." kisha atakutana nae atamuuwa kwa mkuki wake. Wafuasi wake watakimbia wakifukuzwa na Waislamu, ambao watawauwa, na miti na mawe yatasema, 'Ewe Mja wa Allaah kuna Yahudi nyuma yangu-njoo umuuwe!" ila mti wa GHARQAD (BUCKTHORN) kwa kuwa ni miongoni mwa miti ya mayahudi.

Ifuatayo Ni Baadhi Za Hadeeth Kuhusu Kifo Cha ad-Dajjaal Na Wafuasi Wake

Amesema Abdullaah Ibn 'Amr (رضي الله عنه): "Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: "ad-Dajjaal atajitokeza katika Ummah wangu na atakaa arubaini ..., kisha Allaah atamtuma Eesa (عليه السلام) anaefanana na 'Urwah ibn Mas'ood, atamfukuza na atamuuwa." **[Muslim no. 5233]**

Majma' ibn Jaariyah al-Ansaari (رضي الله عنه) alisema: 'Nilimsikia Mtume (صلي الله عليه وسلم) akisema: "Mwana wa Mar'yam atamuuwa ad-Dajjaal katika mlango wa Ludd" **[Ahmad no. 14920 na Tirmidhi no. 2170]**

[Muslim no. 5228- alihadithia hadeeth ndefu kutoka kwa al-Nawwaas Ibn Sam'aan (رضي الله عنه) kuhusu ad-Dajjaal ndani yake, kuja kwa Eesa (عليه السلام) na kumuuwa kwake ad-Dajjaal imetajwa. Katika hadeeth hii Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: "...kila kafiri atakae isikia harufu ya Eesa (عليه السلام) atakufa na manukato yake yatafika umbali wa atakavyo ona. Kisha atamtafuta yeye (ad-Dajjaal) mpaka apambane nae katika mlango wa Ludd, ambapo atakapomuuwa."

Imaam Ahmad kutoka kwa Jaabir ibn Abdillaah (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: "ad-Dajjaal atajitokeza katika wakati ambapo kujitolea katika Dini kutafifia na ilmu kupunguwa...Kisha Eesa ibn Mar'yam atateremka muda mchache kabla ya alfajiri, na atawaita watu, akisema: 'Enyi watu, ni jambo gani linalowazuiya nyinyi kutoka dhidi ya muovu huyu mrongo?' Watasema, 'Mtu huyu ni jinni.' Kisha watatoka. Watakapomfikia Eesa ibn Mar'yam, wakati wa swala utakuwa umeingia, kutaqimiwa, na ataambiwa (Eesa): 'Tuswalishe Ewe Ruhu-llaah.' Atasema: 'Wacheni Imaam wenu atuongoze kwenye swala.' Baada ya kuswali alfajiri watakwenda nje kupambana na ad-Dajjaal, na watakapomuona mrongo huyo, ataanza kuyayuka kama chumvi kwenye maji. 'Eesa atamuendea na amuuwe. Hata Miti na mawe yataita: "Ewe Ruhu-llaah hapa yuko Yahudi!' na hakuna atakaebaki katika wafuasi wa Dajjaal, wote watauawa**" [Ahmad no.14426].**

Atakapo uawa, fitnah yake itakuwa imekwisha. Allaah atawaokowa wale walio mwamini na kujiepusha na uovu wake na uovu wa wafuasi wake katika mikono ya Ar-Ruh na Neno lake (Allaah), Eesa ibn Mar'yam (عليه السلام) na wafuasi wake waumini.